

HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA RUKWA:

FAX: 025 283 0136

SIMU: 025 283 0006



S. L. P. 2,

Namanyere - Nkasi.

KUMB.Na.NKS/DC/A.90/I/VOL III/127

21/04/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Halmashauri ya (W) ya Nkasi imepata kibali cha Ajira mbadala toka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye Kumb Na.FA.170/373/01/35 cha tarehe 24 Machi, 2021 ili kujaza nafasi hizo Mkurugenzi Mtendaji (W) ya Nkasi anakaribisha maombi kwa watazania wenye sifa kama ifuatavyo:-

1.0. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III - NAFASI 2

1.1. SIFA ZA MWOMBAJI:-

1. Awe na Elimu ya kidato cha Nne /Sita
2. Awe amehitimu Mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo :
 - Utawala
 - Rasilimali watu
 - Sheria
 - Maendeleo ya jamii
 - Elimu ya Jamii
 - Usumamizi wa Fedha au
 - Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

1.2. NGAZI YA MSHAHARA

kwa kuzingatia Viwango vya serikali kwa ngazi ya Mshahara TGS B kwa mwezi.

1.3. MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya kijiji.
- Kuratibu Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali ya kijiji
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza

mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.

- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za kijiji.

1.4. MASHARITI YA JUMLA

- Awe Raia wa Tanzania
- Awe na Umri wa Miaka 18 hadi 45
- "Testimonials, Provisional Results, Statement of Result " na hati za matokeo kidato cha Nne na Sita (Form IV na VI Result Slip) HAVITAKUBALIWA.
- Waombaji waliosoma Nje ya Tanzania waakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU)
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- Uwasilishaji taarifa za sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua Stahiki za Kisheria
- Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano.

1.5. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:

Kila muombaji wa kazi awasilishe barua iliyoandikwa kwa mkono ikiambatana na :-

- Wasifu Binafsi (CV)
- Vivuli vya Vyeti vya Elimu na Ujenzi
- Majina matatu ya wadhamini
- Cheti cha kuzaliwa
- Picha mbili za "Passport Size"

1.6. Maombi yote yatumwe kupitia anuani ya Posta kama ifuatavyo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi,
S.L.P 02,
NKASI.

1.7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 03/05/2021 siku ya Juma tatu , muda wa 9:30 alasiri. Aidha, tangazo hili linapatikana kwenye Website ya Halmashauri ambayo ni www.nkasidc.go.tz, Sekretarieti ya Ajira na kwenye Mbao za matangazo.

.....
MISSANA K.KWANGURA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NKASI

MR. MISSANA K. KWANGURA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
NKASI